

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

Simu Nambari: 2152532/3

Baruapepe: cg@dcea.go.tz

Tovuti: www.dcea.go.tz

Nukushi: 2152820



8Barabara ya kivukoni

S.L.P. 80327

Dar es Salaam

Tanzania

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

KUKABIDHI KEMIKALI KWA AJILI YA KUTENGENEZA VITAKASA MIKONO

Dar es Salaam, 18 April 2020:

Serikali imekabidhi jumla ya lita 170,000 za kemikali aina ya Ethanol (ethyl Alcohol) kwa mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam kwa ajili ya kutengenezea vitakasa mikono ili kukabiliana na janga la ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona (covid 19). Kemikali zilizokabidhiwa zilikamatwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kutokana na kuingizwa nchini kinyume na sheria.

Kufuatia ukiukwaji huo wa Sheria ya Usimamizi na Udhhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani namba 3 ya mwaka 2003, kemikali hizo zilizuiliwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kushirikiana na vyombo vingine vya udhibiti wa kemikali. Kufuatia kukamilika kwa taratibu za kisheria, serikali imeamuru kemikali hizo zigawiwe viwandani kwa ajili ya kutengenezea vitakasa mikono ili kusaidia kupunguza gharama za bidhaa hiyo kwa wananchi.

Kemikali bashirifu ni kemikali zenye matumizi ya kawaida katika kutengeneza bidhaa mbalimbali viwandani lakini kemikali hizo zikichepushwa huweza kutumika

kutengeneza dawa za kulevya. kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali jedwali namba 7, udhibiti wa kemikali hizi umewekwa kuanzia hatua ya ununuzi, usafirishaji, uhifadhi na utumiaji. Aidha, kemikali hizi zinaweza kuzalisha sumu ambazo zinaweza kuhatarisha afya na kuchafua mazingira.

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya inawaomba wananchi kuendelea kuunga mkono juhudi na maagizo ya serikali ili kuepusha maambukizi zaidi ya virusi hivyo.

Imetolewa na,



Florence Khambi.

Mkuu wa kitengo cha Mawasiliano

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.